# NOMINO MPYA ZINAZOHUSU WATU KATIKA KISWAHILI

N.V. Gromova

Baada ya nchi za Afrika Mashariki kujipatia uhuru wao lugha ya Kiswahili ilianza kutumika zaidi katika nyanja na fani zote za shughuli za kiuchumi, kijamii na za kiutamaduni zilizoendeshwa na mataifa ya kanda hiyo. Umma wa watu hasa watu wa tabaka la chini walijiingiza katika shughuli mbalimbali za viwandani, mashirika ya kijamii, jumuia nyingi n.k., zaidi ya hayo wengi wao walianza kushiriki katika kuiongoza nchi kuanzia mitaani hadi serikalini; tena, mawasiliano na mahusiano kati ya watu wa mataifa mbali mbali yalianza kutawaliwa na watu wa kawaida au wanyonge wazungumzao Kiswahili. Hayo yote yalisababisha ukuzaji mkubwa na wa haraka wa nomino zinazowahusu watu katika lugha ya Kiswahili.

Kama inavyojulikana nomino zinazowahusu watu au majina ya watu hushika nafasi kubwa katika msamiati wa kila lugha sanifu kwa sababu binadamu anapewa uzito mkubwa katika mazingira yake, yeye ni mtenda na mtendwa, sifa zake tofauti zinazotokana na uhusiano wake na watu wengine, vitu na maumbile zinaelezwa kwa maelfu ya maneno. Mathalani, msamiati wa lugha ya Kirusi una nomino zinazowahusu watu zisizopungua asilimia 10 (Shkataova, 1986:37).

Nomino zinazohusu watu katika lugha za Kibantu zinajumuishwa ndani ya ngeli maalum ya majina. Kufuatana na uainishaji wa ngeli uliofanywa na C. Meinhof au M. Guthrie, hii ni ngeli ya kwanza inayounganisha majina mbalimbali ya binadamu. Ngeli hii ina tabia yake ya pekee: semantiki yake ni ya aina moja tu kinyume cha ngeli nyingine ambazo zina kiini au kitovu maalum cha kisemantiki lakini wakati huo huo zinaunganisha nomino zenye maana tofauti zisizolingana na kile kiini chake cha kisemantiki. Tuchukue mfano wa ngeli ya 3. Ngeli hii huwa inaelezwa kama "ngeli ya miti na mimea" kwa kutegemea kiini chake cha kisemantiki. Kwa upande huu, ngeli ya

kwanza hushika nafasi mahususi katika mfumo wa nomino za Kiswahili: semantiki ya kimsamiati ya maneno yaliyomo katika ngeli hiyo ni aina moja tu: [1]/, majina yote yenye kiambishi awali m-/mw-[2] ni nomino zinazohusu watu watupu tu[3/].

Madhumuni ya makala hiyo ni kuchambua nonimo mpya za ngali ya kwanza, hasa maumbo yao na ruwaza zinazotumika katika kujenga nomino mpya zinazowahusu watu.

Majina mapya ambayo kuibuka kwao kumesababishwa na sababu zisizo za kiisimu ni asilimia kubwa ya nomino za watu. Tukilinganisha kamusi mbili thaniya za Kiswahili yaani ile kamusi kubwa ya Johnson ya mwaka 1939 na kamusi ya wanajopo Warusi ya mwaka 1987, tunaweza kupata majina ya watu yenye idadi 738 katika kamusi ya kwanza, jumla ya majina 1395 ya watu yaliyomo katika kamusi ya pili. Hivyo kwa muda wa takriban nusu karne maneno mapya yahusuyo watu yalijitokeza kwa wingi, idadi yao iliongezeka karibu maradufu.

Uchambuzi wa nomino zinazohusu watu unadhihirisha kuwa nusu karne nyuma, maneno yaliyokuwa mengi zaidi yalikuwa ni yale majina ya mnyambuliko (maneno 611) yaliyojengwa kutokana na vitenzi vizalia vya Kibantu na vitenzi vilivyotoholewa kutoka Kiarabu. Majina ya mnyambuliko yaliundwa kwa njia ya kupachika viambishi awali katika mzizi au shina la kitenzi, yaani:

*Ka + kitenzi kizalia*    *au*    *Ka + kitenzi cha mkopo*

| | |
|---|---|
| *m-cheza* | *m-bashiri* |
| *m-pend-wa* | *m-dai-wa* |

au kwa matumizi ya kiambishi awali pamoja na kinyambulishi kingine kinachowakilishwa na kimojawapo cha viambishi tamati:

*Ka + kitenzi kizalia + Kt*    *au*    *Ka + kitenzi cha mkopo*

*m-sem/a/-i*
*m-chunga-ji*
*m-pamba/a/-e*
*m-f/a/-u*
*m-danganyi/a/-fu*
*m-samehe-ji*
*m-badhiri-fu*

Ikumbukwe kwamba zipo ruwaza tofauti zinazotumika katika kunyambulisha majina ya watu kutokana na vitenzi zalia na vitenzi vya Kiarabu. Aghalabu majina yakiundwa kutokana na vitenzi vya Kiarabu yanafuata ruwaza Ka + kitenzi, hasa mzizi wa kitenzi, au Ka + kitenzi + Kt ambapo kiambishi tamati kinawakilishwa na moja ya mofimu -fu/-vu. Neno moja tu lilikuwa limejengwa kwa kutumia kiambishi ngeli ya kwanza, mzizi wa kitenzi cha Kiarabu na kiambishi tamati -ji (m + samehe +ji). Viambishi tamati vyenye muundo wa irabu moja tu yaani -i, -o, -e, -u havikutumika katika mnyambuliko unaobadilisha kitenzi cha Kiarabu kuwa nomino. Inayumkinika kuwa havikutumika kwa sababu muundo wa vinyambulishi hivi ni sawa na miishio ya vitenzi vya Kiarabu (ling. -rud, -samehe, -jibu). Vitenzi vya Kiarabu vilivyoambikwa viambishi tamati vya Kiswahili (kimoja au zaidi) vinatumika sawa na vitenzi vizalia yaani vina nafasi ya kuambatana na viambishi tamati vinavyobadilisha kitenzi kiwe nomino.

Majina yasiyonyambulika kutokana na vitenzi yaliyomo katika ngeli ya watu yalichukua sehemu iliyo ndogo, takriban sehemu ya sita ya nomino zote zihusuzo watu. Kati ya majina hayo yamo :

(i) majina mazalia,

(ii) majina ya mnyambuliko unaobadilisha vivumishi kuwa nomino au unaobadilisha maana ya majina ya ngeli nyingine,

(iii) majina ya mkopo toka lugha ya Kiarabu.

Kila fungu lina maneno machache tu kiasi tungeweza kuyaorodhesha:

(i) Majina mazalia ambayo ni msingi halisi wa msamiati yanawakilishwa na nomino za watu zifuatazo: mfalme, mchawi, mhenga, mjane, mjoli, mke, mume, mtoto, mvuli na mengine machache.

(ii) Nomino chache zihusuzo watu ni za mnyambuliko unaobadilisha vivumishi kuwa nomino. Tunaweza kuyabainisha kama vivumishi-majina, kwa mfano: mzee <-- -zee, mkongwe <-- -kongwe, mkale <-- -kale, mkubwa <-- -kubwa, mdogo <-- dogo n.k.

Nomino zinazoingia katika ngeli nyingine zinaweza kutumika zikiwa mzizi / shina la unyambulikaji wa majina ya watu: mkoo <-- koo (ngeli ya 5/6), mdeni <-- deni (ngeli ya 5/6), msiri <-- siri) ngeli ya 9/19), mchumba <-- chumba (ngeli ya 7/8) n.k. Maneno ya kijiografia kama yale majina ya miji, nchi au visiwa, yanaweza kunyambulisha nomino za watu hasa wenyeji wa miji, nchi au visiwa vilivyohusika: mreno <-- Ureno, mfaransa <-- Ufaransa, mnasarani <-- Nasarani, mngazija <-- /visiwa vya/Ngazija, myunani <-- Uyunani na mengineyo. Kama inavyoonekana hapo juu, majina ya aina hii yameundwa kwa kupachika kiambishi ngeli peke yake (m+zee) ama kwa kubadilisha kiambishi ngeli ya neno lililotumika kama mzizi wa unyambulikaji kwa kiambishi cha ngeli ya kwanza (m + /u/reno). Kwa nadra tunaweza kuona viambishi awali viwili pamoja au viambishi awali maradufu : mchumba <-- m + ch+ umba.

(iii) Fungu la majina ya mkopo wa ngeli ya kwanza linaunganisha majina yafuatayo ya watu: mwalimu, muhibu, mwumini, mutribu, mwislamu n.k. Nomino hizo za mkopo, kusema kweli hazina viambishi awali ila wazungumzaji wa Kiswahili wanatenga kiambishi ngeli mu-/mw- kwa kutegemea ufanano (analogy) na muundo wa majina mazalia ya Kiswahili, ling. neno la Kiarabu "muallim" lenye silabu mu-al-lim na neno la Kiswahili "mwalimu" lenye kiambishi ngeli ya kwanza (uwingi wake ni waalimu).

Nomino zinazohusu watu huwa yanagawanywa katika mafungu sita ya kisemantiki:

(i) yale yanayoeleza hali ya kiume au ya kike ama hali ya nasaba (udugu wa nasaba) pamoja na umri wa mtu fulani: mke, mume, mtoto, mvulana n.k.

(ii) yale yanayoeleza mahali mtu anakotoka au kabila/taifa lake: Mngazija, Mjerumani, Mswahili, Mwarabu, Mhindi n.k.

(iii) yale yanayobainisha shughuli au kazi za mtu: mchungaji, mfasiri, mlimaji, mwashi, mwuzaji n.k.

(iv) yale yanayoeleza wadhifa wa mtu, hali yake ya kijamii, upendeleo wake wa itikadi fulani, dini, chama n.k.: mkulima, mtumishi, mfanyi, mkristo, mwislamu;

(v) yale yanayoeleza tabia hasa za mtu fulani: mjinga, mwongo, mkaidi, mdadisi, mnyamavu n.k.

(vi) yale yanayoeleza kifaa au kitu mtu anachotumia katika shughuli zake ama kukitengeneza: mshona viatu n.k.

Ni fungu la kwanza tu linalojumuisha maneno mazalia, mafungu mengine kama kawaida yana nomino za mnyambuliko zilizoundwa kutokana na kanuni zilizotajwa juu (Ka + kitenzi/kivumishi/nomino, Ka + kitenzi + Kt) au kwa kuyaunganisha maneno mawili. Ikumbukwe kuwa katika kamusi ya Johnson yanapatikana maneno pacha machache sana yaani maneno yafuatayo tu: mlariba, mla watu na mwanasesere.

Kwa muda wa miaka 50 iliyopita msamiati wa Kiswahili umeendelea na kukua sana. Yalikuwa yamezalishwa maneno mengi mapya yanayowahusu watu. Mafungu ya kimsamiati na ya kisemantiki ya nomino za watu yalibaki yale yale tu kwa sababu uainishaji wa namna hii wa majina ya watu unahusu lugha zote (ingawa tunaweza kuyagawa majina hayo katika mafungu mengi zaidi). Kile kilicho kipya katika kuzalisha nomino za

watu ni matumizi ya mbinu mpya.

Kabla ya yote inapaswa kutilia mkazo upanuaji wa mipaka ya maana ya nomino za watu zilizotumika hapo awali. Aidha, tuchukue mfano wa neno "mteja." Nomino hiyo yenye maana ya kwanza "mtu anayekwenda kwa mganga kwa ajili ya kuaguliwa" ilipewa maana nyingine zaidi yaani "mtu anayekwenda kwa mtu k.v. daktari au wakili au shirika n.k. kutimiziwa haja zake" (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 194-195). Neno "mchokozi" lenye maana "mtu mwenye kuleta ugomvi; mkorofi" linapata maana ya "agressor"; nomino "mfadhili", yaani "mtu anayemfanyia wema mkubwa mtu mwingine; mtu mkarimu" katika matini ya kiuchumi inapata maana mpya ya kiistilahi "donor"; nomino "mgeni" yenye maana yake ya kwanza "mtu asiye na ujuzi maalum (kwa mfano "mgeni wa kazi", "mgeni wa lugha") n.k. Maneno mapya ya aina hii yanahifadhi maumbo yao ya zamani, lakini ujazo wake mpya wa kisemantiki unasababisha uhusiano mpya wa kimsamiaci ambao haukuwezekana kutokea kwa maneno yenye maana ile ya zamani tu. Hayo yanaonekana wazi tukiangalia mafungu ya maneno yanayowakilisha dhana moja, kwa mfano nomino "mfuga" (mtu anayewaweka wanyama kwa ajili ya kuwatunza kwa biashara au chakula) inapewa maana finyu ndani ya fungu hili la maneno "mfuga nyuki"; tena, "mchuuzi" lenye maana "mtu afanyaye kazi ya biashara ya kuuza vitu" likiunganishwa na maneno mengine ndani ya fungu lifuatalo "mchuuzi asimamiaye watu wa nje" likawa istilahi "comprador."

Zaidi ya upanuzi wa maana ya nomino, msamiati wa Kiswahili huongezeka kwa maneno mapya ya mnyambuliko. Sawa na nusu karne nyuma, siku hizi ruwaza zinazopendelewa kutumika katika kujenga majina mapya ni zile ruwaza za jadi yaani Ka + kitenzi na Ka + kitenzi + Kt.

Tukiangalia nomino zilizojengwa kwa kutegemea ruwaza ya kwanza tunaona bayana idadi kadhaa ya jozi za nomino zenye maana "mtenda" na "mtendwa." Kimofolojia ina maanisha kwamba kitenzi cha kwanza kiwe katika kauli ya kutenda na cha pili kiwe katika kauli ya kutendwa, kwa mfano: mwajiri - mwajiriwa, mkosa -

mkoswa, mtahini -mtahiniwa, mhoji -mhojiwa, n.k. Mara nyingi nomino iliyokuwemo tayari katika msamiati wa Kiswahili yenye maana ya kisemantiki ya "mtenda" inapata nomino nyingine ya jozi yake yenye maana ya "mtendwa", mathalan mfadhiliwa, mtesa - mteswa, mtawala -mtawaliwa (kati ya mifano hiyo nomino za upande wa kushoto zenye maana ya "mtenda" ziliorodheshwa katika kamusi ya Johnson). Kwa vile kila kitenzi katika lugha ya Kiswahili kinaweza kuwa katika kauli ya kutendwa, mtindo wa unyambulikaji Ka + kitenzi cha kauli ya kutendwa unaweza kuzalisha maneno mengi mapya yahusuyo watendwa.

Ruwaza ile ya Ka + kitenzi + pia inazalisha idadi kubwa ya nomino mpya: mbadilishaji (m + badilisha + ji), mchomoaji (m + chomoa + ji), mfungaji (m + funga + ji), mchambuzi (m + chambua + i[4]/), mjivuni (m + jivuna + i) n.k. Itiliwe mkazo kuwa vinyambulishi -ji na -i vinatumika zaidi kuliko vingine -e, -o, -u vikiambikwa kwenye mzizi wa kitenzi au shina la kitenzi cha mnyambuliko. Kitenzi cha kauli ya kutendwa tu hakiwezi kuambikwa kiambishi tamati -i ijapokuwa kinaweza kubeba kiambishi tamati -ji: mgandamizaji - mgandamizwaji, mlipaji -mlipwaji. Kile kiambishi tamati -ji kuwekwa nyuma ya vitenzi vya mkopo vya Kiarabu. Kauli hii inapingana na ile ya wachunguzi waliotangulia kwamba kutotumiwa kwa viambishi tamati -ji/-i katika kunyambulisha majina kutokana na vitenzi vya Kiarabu kunaonyesha wazi kwamba vitenzi hivyo havitoholewi ipasavyo na lugha ya Kiswahili. Mifano inayotetea na kuihami kauli yangu ni "msameheji" (neno hili limo katika kamusi ya Johnson), "mbuniji" (maneno hayo mawili yalipatikana katika magazeti ya Kiswahili, tena yaliorodheshwa na Kamusi ya Kiswahili-Kirusi). Mifano hiyo inathibitisha tena jukumu na hadhi kubwa ya mfumo wa kimuundo/kimaumbo wa lugha ya Kiswahili unaoongoza uhusiano na kazi ya vipashio vya lugha. Wakati huo huo hadhi ya subsystem ya Kiarabu ikashuka na ikawa finyu zaidi[5]/.

Nomino za mnyambuliko unaobadilisha majina ya ngeli mbali mbali yawe ya ngeli ya kwanza zinaendelea kupanuka. Sehemu inayochukuliwa na nomino mpya

ikaongezeka. Ruwaza ile ya Ka + nomino inatumika sana katika kuzalisha majina ya watu kufuatana na nchi, mji, mkoa n.k. wanakotoka, kwa mfano: Mchina, Mdenmarki, Mganda, Mgoa, Mrumi, Mmisri, Mwitalia, n.k. Haiwezekani kuorodhesha majina yote ya wakazi wa mahali fulani. Kadiri uhusiano na mawasiliano ya kimataifa ya wazungumzaji wa Kiswahili yanavyoendelea kupanuka, lugha ya Kiswahili imejazwa na maneno mengi ambayo hayakuwamo katika lugha hii miaka 50 iliyopita. Wakitafsiri dhana hiyo wanajopo wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu wanatumia kisawe "mtu mwenye asili ya..." au "mwenyeji wa..". Kabla nomino mpya haijaotesha mizizi katika matumizi ya wazungumzao Kiswahili, nomino mpya na kisawe chake ambacho ni fungu la maneno, vinatumika sambamba kama vile "Wasumbiji" na "wenyeji wa Msumbiji".

Ruwaza ile ile Ka + nomino inazalisha majina ya watu ambayo yanaeleza hali au tabia zao kufuatana na maana ya nomino asilia ambayo ni msingi wa mnyambuliko: mjiguu <-- jiguu "mwenye miguu mikubwa", mlimi <-- ulimi "mtu mwenye tabia ya kusemasema sana", mkunguni <-- kunguni "mtu mvivu anayetega wakati wa kufanya kazi; mtu asiyependa kufanya kazi", mgozi <-- ngozi "mbaguzi rangi", mkweli <-- kweli "mtu anayesema ukweli," mchoyo <-- uchoyo "mtu mwenye tabia ya kunyima" n.k.

Ruwaza ile ile Ka + nomino inatumika pia katika kunyambulisha majina ya watu kutokana na shughuli au kazi wanazofanya: mdiplomasi <-- diplomasi, mfizikia <-- fizikia, mbunge <-- bunge, mjiolojia <-- jiolojia, mtakwimu <-- takwimu; kufuatana na itikadi au dini yao au uanachama wa shirika ama jumuia fulani: mjamaa, mkomunisti, mkatoliki, mprotestanti, mmisionari n.k.

Idadi ndogo ya majina mapya yalibuniwa kutokana na vivumishi vya sifa. Pengine sababu ya kuwa na kiasi kisicho kikubwa cha nomino mpya za aina hii ni idadi ndogo ya vivumishi vyenyewe vya sifa katika lugha ya Kiswahili. Nomino mpya za aina hii ni kama zifuatazo: mchache <-- -chache "mtu anayekosa kitu" (mchache wa subira), mbora <-- -bora "mtu anayejifikiri ni bora

kuliko wengine" n.k.

Kamusi zilizotolewa hivi karibuni zinaorodhesha majina mengi mapya ya watu ambayo ni majina mazalia. Lakini nomino hizo, kusema kweli, hatuwezi kuziita mpya tukiangalia maana yao. Hayo ni maneno mazalia yaliyoponyoshwa tu katika kamusi ya Johnson au pengine hayakuingizwa kwa makusudi tu. Ni maneno yafuatayo: mdema "mtoto mwenye umri wa miezi 9 hadi miaka miwili", mchuchu "mpenzi", mmula "mtu", mkomba "mlevi", mcheja "baba au mama wa mke au mume", mkembe "mtoto mdogo mwenye umri baina ya mwaka mmoja na miaka sita", mkiwa "mtu aliyefiwa na mama, baba au ndugu", mkoi "mtoto wa ndugu wa kiume wa baba mzazi, shangazi au mjomba", mkoloni "mtu anayetawala katika nchi ambayo si yake, mndeva "mtu ambaye ni kiongozi wa jamii yake, balozi wa kijiji", mteke "mtu mwoga" mtukuu "mtoto wa mjukuu", muwele "mgonjwa" n.k.

Katika kamusi ya Johnson maneno pacha ni machache tu, lakini kamusi za kisasa zinaorodhesha maneno mengi mapya yaliyoundwa kwa kutegemea ruwaza mbili:

(i) Nomino (ya ngeli ya kwanza iliyonyambulishwa kutokana na vitenzi) + Nomino (isiyo ya ngeli ya kwanza);

(ii) Nomino (ya ngeli ya kwanza ambayo ni neno zalia) + Nomino (isiyo ya ngeli ya kwanza).

Ruwaza ya kwanza inaweza kuzalisha nomino zinazowahusu watu kwa kuelezea kitu wanaochokishughulikia. Nomino ya mnyambuliko inayochukua nafasi ya kwanza katika neno pacha imeundwa kwa kupachika kiambishi ngeli peke yake (bila ya kiambishi tamati). Maana yake ya kisemantiki inaelezwa hasa na nomino ya pili:

*kamari*
*sarakasi*
*ngoma*
*mcheza* + *sataranji*

*sinema*
*tarumbeta n.k.*

Tahajia ya manenopacha yenye umbo kama hilo si ya kudumu bado, maneno ya aina hiyo yanaweza kuandikwa pamoja: mpigambizi, mfanyakazi au neno moja moja: mpiga chapa, mfanya kazi. Lakini haya yakiandikwa moja moja yanawakilisha dhana ya pekee na vipashio vingine haviwezi kujiingiza kati ya sehemu hizo mbili za neno pacha. Hii ina maanakwamba mchangamano wa majina mawili huunda neno lenye maana moja. Manenopacha (au majina mchangamano)' ya aina hiyo yana maneno mawili ambayo kila moja kati yao linahifadhi uhuru wake wa kuchangamana na maneno mengine: angalia mifano iliyotolewa juu yenye kipashio "mcheza", ambayo ni sehemu ya kwanza ya nenopacha. Tena, sehemu ya pili ya nenopacha kwa upande wake ina nafasi ya kuchangamana na maneno tofauti, linganishi mfululizo huo wa manenopacha:

*mpiga*
*mpenda + ngoma*
*msoma*
*mcheza*

Ikihitajika tu ruwaza hiyo inawezesha kuunda majina mapya ya watu ambayo idadi yao haipunguzwi katika mawasiliano ya watu.

Katika ile ruwaza ya pili, ambayo sehemu yake ya kwanza ni nomino zalia, kama kawaida nomino hiyo inawakilishwa na jina "mwana." Likichangamana na nomino nyingine linazalisha nomino za watu zinazoelezea itikadi yao, uanachama, shughuli, kazi n.k. yaani maneno pacha ya aina hii yanapatikana katika kila la mafungu 6 ya kisemantiki yaliyotajwa juu, kwa mfano: mwanachama, mwanafalsafa, mwanaharakati, mwanaitikadi, mwanakifaru, mwanambio, mwanamapinduzi, mwanariadha na mengine mengineyo Idadi yao ni kubwa na haiwezekani kuyaorodhesha yote katika kamusi.

Nafasi ya kwanza inaweza kuchukuliwa pia na neno "mwenye" ambalo ni shida kidogo kueleza etimolojia yake. Likiingia katika kundi la maneno au sentensi linapata upatanisho wa kisarufi ulio sawa na viwakilishi (pronoun): jambo lenye maana, maziwa yenye samaki, nyumba zenye madirisha n.k. (ling.: hili, yale, zangu). Lakini katika ngeli ya kwanza neno hilo linapatanishwa si kama kiwakilishi (mtoto yule wangu) bali kama kivumishi (mtoto mzuri mwenye...). Hatutajadili hapa swali juu ya aina ya maneno ambayo hilo "mwenye" huingia ndano yao. Inapaswa kusema tu kwamba katika lugha ya kisasa ya Kiswahili inawezekana kuumba mkururo mrefu wa manenopacha yenye "mwenye" katika nafasi ya kwanza. Nafasi ya pili hushikwa na neno lolote la ngeli tofauti, kuanzia ngeli ya kwanza hadi ngeli ya ku-: mwenye hatia, mwenye hisa, mwenye deni, mwenye kufilisika, mwenye kudhamini, mwenye kujitwaza n.k.

Kwa kuhitimisha lazima kusisitiza kwamba nomino mpya zinazowahusu watu huonyesha wazi kwamba ruwaza za kimapokeo au ruwaza kongwe za kuunda majina zinatumika sana siku hizi. Wakati huo huo uzito wa manenopacha huongezeka mno.

*Vidokezo*

1. Hapo ningependa kueleza kwa kifupi maoni yangu kuhusu vigezo vya kuainisha ngeli za nomino katika lugha ya Kiswahili. A. Gibbe katika makala yake ya "Uchambuzi wa nomino za ngeli ya kwanza katika Kiswahili" anasisitiza kwamba ngeli hiyo inaunganisha nomino zote zenye viambishi awali mu-, mw-, wa-, w-, ki-, vi-, ma-, mi- na nomino nyingine zisizotumia viambishi awali hata kidogo. Nomino hizo zote "zimeweza kuainishika katika ngeli ya kwanza kwa kutumia kiambishi cha kitenzi a-"/uk. 245/. Bila shaka, maelezo hayo ni ukweli usiopingika, lakini kwa upande mwingine kigezo kinachotumiwa na A. Gibbe ni (i) kigezo tata kwa sababu nomino zinazohusiana na ngeli hiyo hazina kile kinachoziainisha kimofolojia yaani kiambishi ngeli cha aina moja. Tukifuata kigezo hiki ambacho ni cha kisemantiki kwa jumla (nomino

zinazowahusu watu, wadudu, wanyama, ndege, malaika, shetani na Mungu /uk. 247), tuziitaje ngeli ya 5/6 au Li-/YA-? Je, ni ngeli ya nomino zinazohusu mawe, maji, maziwa, viungo vya mwili, matunda n.k.?
(ii) A. Gibbe mwenyewe anakaribia kutatua swali hili lililomkabili akitumia kigezo cha udhananishaji "kigezo muhimu kinachotumika kubainisha nomino kuwa ni za ngeli ya kwanza ni uwezo wa kukata roho" /uk.247/. Wachunguzi waliotangulia walielezea kigezo hikihiki kama ndicho kinachobainisha kategoria mpya inayoibuka katika Kiswahili (sawa na lugha nyingine za Kibantu lakini sio zote) yaani kategoria ya uhai ambayo kionyeshi chake ni upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya kwanza (ling. na kategoria ya locative ambayo kionyeshi chake ni kiambishi tamati -ni na upatanisho wa kisarufi wa ngeli za pa-, ku- au mu-) /Meinhof; Gromova; Okhotina/.

2. Kiambishi ngeli m- hutumika mbele ya konsonanti inayoanzia mzizi wa nomino, mu- aua mw- mbele ya irabu ya kwanza ya mzizi, kwa mfano: m-semaji, mu-uzaji = mw-uzaji (ingawa Kamusi ya Kiswahili Sanifu inasisitiza muundo mu- mbele ya irabu /u/: muungwana, muuza, muungamaji, muumini n.k.), mw-ombaji, mw-amuzi, mw-imbaji, mw-ezekaji.

3. Katika ngeli ya kwanza kuna nomino mbili tu zisizowahusu watu. Nomino hizo ni "mdudu" (jina zalia) na "mnyama" ambalo limeundwa kutokana na neno "nyama" (ngeli ya 9/10) + kiambishi awali maradufu cha ngeli ya kwanza m-.

4. Mabadiliko ya kimofonolojia yanayoibuka katika mipaka kati ya mofimu na mofimu yameelezwa katika makala yahusuyo unyambulikaji wa nomino /Gromova, Okhotina/. Hapa nataka kueleza kauli yangu kwa kifupi tu: ikiwa kiambishi tamati inaanzia na konsonanti hapatokei mabadiliko yoyote (kanuni hii inahusu kiambishi tamati -ji), ikiwa kiambishi tamati kinawakilishwa na irabu yaani -i, -e, -o, -u, hivyo irabu hii inadondosha irabu ya mwisho /a/ ya kitenzi na zaidi ya hayo kiambishi tamati chenye muundo wa irabu peke yake kinaweza kuathiri konsonanti inayotangulia ya

zaidi ya hayo kiambishi tamati chenye muundo wa irabu peke yake kinaweza kuathiri konsonanti inayotangulia ya mzizi/shina la kitenzi, ling. mifano ifuatayo: m + pika + ji --> mpikaji, m + pika + i --> pik/a/ + i --> mpishi (k --> sh), m + chomoa + ji --> mchomoaji, m + chomoa + i --> m + *chomol/a/ + i --> mchomozi (l --> z).

5. Tunaweza kutaja Mifumo midogo ya Kiarabu iliyomo katika mfumo wa Kiswahili: (i) ya kifonetiki/kifonolojia (konsonanti dh, th, gh n.k. ambazo wazungumzaji wa kawaida wanajaribu kubadilisha matamshi yao yawe z, s, g); (ii) ya kimofolojia (kiishilizi cha nomino na vitenzi : furaha - furahi, maumbo yao: athari -athiri; kanuni za unyambulishi wa nomino na vitenzi: -piga + na --> pigana, lakini -samehe + ana --> sameheana n.k.); (iii) ya kisintaksia (vivumishi vya mkopo vya kiarabu havifuati kanuni za upatanisho wa kisarufi: mtu mwema, lakini mtu safi n.k.).

**MAREJEO**


Gibbe, A. 1983 Uchambuzi wa nomino za ngeli ya kwanza katika Kiswahili. Makala za Semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kiswahili". Jz. 1,

Gromova, N.V. 1966 Chasti rechi v yazikah Bantu i printsipi ikh razgranicheniya. Moscow,

Gromova, N.V. 1988 Okhotina N.V. Imennoye otglagolnoye slovoobrazovaniye v suahili."Voprosi afrikanskoy filologii", Moscow,

Johnson, F. A 1939 Standard Swahili - English dictionary. Oxford,

K.K.K. 1987 Kamusi ya Kiswahili-Kirusi. Moscow,

Kapinga, M.C. 1983 Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam,

Okhotina, N.V. 1989 Tendetsii vozniknoveniya innovatsionnikh kategoriy v nadetnicheskikh yazikakh Bantu. "Voprosi yazikoznaniya", Moscow,

Meinhof, C. 1948 Grundzuege einer vergleichended Grammatik der Bantusprachen. Hamnburg,

Shkatova, L.A. 1986 Razlichniye stepeni terminologizatsii naimenovaniy lits. "Sovremenniye problemi russkoy termonologii." Moscow,

TUKI 1981 Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam, Nairobi,